**Jina la Shule:** SHULE YA SEKONDARI MUZYE **Jina la Mwalimu:** MKANDAMA ISA

**Kidato:** Kidato cha Kwanza **Tarehe:** 15/1/2025

**Muda:** Saa 2:00 – 3: 20

**Somo:** ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

| Idadi ya Wanafunzi | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Waliosajiliwa** | | | **Waliohudhuria** | | |
| **Wasichana** | **Wavulana** | **Jumla** | **Wasichana** | **Wavulana** | **Jumla** |
| **30** | **30** | **60** | **30** | **25** | **55** |

**Umahiri Mkuu:** Kumtambua, kumpenda, kumtukuza na kumsifu Allah (S.W)

**Umahiri Mahususi:** Kutambua uwepo wa Allah (S.W) na sifa zake

**Shughuli Kuu:** Kufafanua dhana ya Elimu kwa mtazamo wa Uislamu

**Shughuli Mahususi:**

(i) Kutoa maana ya elimu na kutaja sifa za mtu aliyeelimika kwa mtazamo wa Uislamu
(ii) Kueleza chanzo cha elimu na umuhimu wa elimu kwa mtazamo wa Uislamu
(iii) Kubainisha mgawanyo wa elimu katika Uislamu
(iv) Kufafanua umuhimu wa Elimu ya Dini ya Kiislamu na mahusiano yake na masomo mengine.

**Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji:**

(i) Kitabu cha kiada kidato cha kwanza
(ii) Tafsiri ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy
(iii) Bango kitita
(iv) Projecta, simu janja na kishikwambi.

**Rejea:** TISTA (2024). *Elimu ya Dini ya Kiislamu, Kitabu cha mwanafunzi kidato cha kwanza*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania

**Mchakato wa Ufundishaji na Ujifunzaji**

| Hatua | Muda (Dakika) | Shughuli za Ufundishaji | Shughuli za Ujifunzaji | Vigezo vya Upimaji |
|---|---|---|---|---|
| **Utangulizi** | Dakika 10 | Kwa kutumia maswali na majibu kuwauliza wanafunzi kueleza dhana ya elimu katika Uislamu | Kujibu maswali kuhusu dhana ya elimu katika Uislamu | Dhana ya elimu imeelezwa |
| **Kuendeleza ujenzi wa umahiri** | Dakika 35 | Kuwagawa wanafunzi katika makundi kujadili dhana ya elimu katika Uislamu kwa kutumia video, kitabu cha mwanafunzi kidato cha kwanza , na kuwasilisha | Kujadili na kuwasilisha dhana ya elimu katika Uislamu | Dhana ya elimu katika Uislamu imewasilishwa |
| **Kubuni** | Dakika 25 | Kuwashirikisha wanafunzi katika makundi kuandika muhtasari kuhusu namna ya kukabiliana na dhana potofu kuhusu elimu na athari zake katika jamii kisha kuwasilisha mbele ya darasa | Kuandika muhtasari kuhusu namna ya kukabiliana na dhana potofu kuhusu elimu na athari zake katika jamii | Muhtasari kuhusu namna ya kukabiliana na dhana potofu kuhusu elimu na athari zake katika jamii umeandikwa |
| **Tathimini** | Dakika 10 | Kutoa zoezi kwa wanafunzi kuhusu dhana ya elimu katika Uislamu na kuwataka waandike majibu katika madftari yao na kubadilishana ili kupata tathmini | Kujibu maswali kuhusu dhana ya elimu katika Uislamu na kubadilishana madaftari | Maswali kuhusu dhana ya elimu katika Uislamu yamejibiwa |

Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania

**Maoni:** Wanafunzi 50 /55 waliweza kufafanua dhana ya Elimu katika Uislamu kutokana na mbinu na zana zilizotumika. Wanafunzi 5 walishindwa kufafanua kwa usahihi mahusiano ya somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu na masomo menginekutokana na mbinu na zana zilizotumika. Hivyo, nitatafuta muda wa ziada na kutumia mbinu na zana tofauti kuwaelekeza na nitaendelea na umahiri mahsusi huu katika kipengele cha dhana ya dini kwa mujibu wa Qur’an na Sunnah kipindi kinachofuata.